CORRUPTION ALMANAC

Integrity Watch (IWa)

ISSN: 022 *Issue No.27. January - March 2012*

Yaliyomo

- Maeneo ya Kumulikwa
- Sh.Trillion 1.7 za Umeme wa Dharura
- Rushwa imepenyeza sehemu takatifu?
- Kinondoni: Huduma za Afya Zazorota katika Lindi la Utajiri.
- Integrity Watch Yazindua Mradi wa Afya
- Kutoka Magazetini n.k

INTEGRITY WATCH

This newsletter is published by **Integrity Watch,**
ESAURP House, Survey Area**, P.O. Box** 35683, Dar es salaam, Tanzania
Tel:+255612253545, **Mobile:** +255-784508007, +255-787809378
Email:info@integrity-watch.com, **Web**: www.integrity-watch.com

Tahariri

Tukomeshe tatizo la rushwa mwaka huu

KATIKA toleo hili la jarida la *Corruption Almanac* tunaangazia tatizo la rushwa nchini na kubainisha baadhiya maeneo ambayo tukitilia mkazo yatasaidia kupunguza tatizo hili nchini. Hayati Baba waTaifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alionya mara kadhaa hasa wakati wa mchakato wa uchaguzi mwaka 1995 kwamba rushwa ni adui wa haki na kwamba serikali inayokumbatia rushwa inawanyima raia wake walio wengi haki, huduma za jamii na maendeleo kwa ujumla.

Mwl alisema rushwa ambayo ilikuwa imekithiri wakati wa Rais wa Awamu yaPili, Bw Ali Hassan Mwinyi ilikuwa inawanyima wanyonge haki, huduma muhimu za jamiii kama vile afya na elimu lakini pia kupoteza-mapatoya serikali.

Mambo mengi aliyoonya Mwl Nyerere wakati wa uhai wake hasa rushwa kushamiri katika serikali na vyama vya siasa hasa Chama Cha Mapinduzi (CCM) tunayashuhudia leo hii kwani rushwa inanyima wanyonge haki zao ikiwemo haki ya kuishi, mahakamani, makazini, huduma mbaya za jamii na upotevu wa mabilioni ya pesa za walipakodi.

Leo hii tunashuhudia habari nyingi katika vyombo vyetu zikieleza tatizo la rushwa kuwa kubwa na kusaba-bisha maafa mahospitalini na hata katika ofisi za serikali. Toka enzi za Rais mstaafu Benjamin William Mka-pampaka leo hii chini ya utawala wa Jakaya Mrisho Kikwete, tatizo la rushwa limekuwa sugu kiasi kwamba limeenea katika Nyanja mbalimbali za nchiyetu.

Rushwa imetawala kwenye siasa za ushindani, serikalini, katika utoaji huduma za jamii, katika michezohasa Ligi Kuu ya Tanzania lakini baya zaidi leo hii ni rushwa kuanza kuonekana kwenye taasisi za dini.

Leo hii Watanzania wenye tuhuma kubwa za rushwa, wafanyabiashara, wachungaji na wengineo wanasaka nafasi za kisiasa katika vyama au serikalini wanajipitishapitisha makanisani na misikitini wakiendesha harambee za kuchangia maendeleo katika taasisi hizo za dini.

Vyombo vya habari vimekuwa na taarifa nyingi za baadhi ya watu hawa ambao wanawania kumrithi Rais Kikwete mwaka 2015 atakapostaafu na kwa hiyo wanatafuta uungwaji mkono na waumini wa dini za aina zote.

Jambo la kuchagua wanasiasa safi na makini katika uchaguzi wa ndani ya vyama au kuongoza dola ni muhimu sana kufuata maadili na ndiyo maanaRais Kikwete ambaye pia ni Mwenyekiti waTaifa wa CCM amewaasa wanachama wenzake kuchagua watu waadilifu kukiongoza chama hicho mwaka huu ilikiweze-kuendelea kushika dola mwaka 2015.

Kama CCM ikipata viongozi safi wa ngazi ya taifa basi nchi yetu itakuwa imepiga hatua kubwa katika kupambana na rushwa kwani ndicho chama kinachoshika dola, kwa hiyo kitakuwa makini katika kuondoa-watendaji wabovu ambao wamesababisha upotevu wa mabilioni ya fedha nchini huku huduma za jamii zikizorota na miundombinu kuchakaa.

Ni matumaini ya*Corruption Almanac* kwamba mwaka huu uchaguzi wa CCM na vyama vingine utaleta ufanisi wa kupambana na rushwa katika Nyanja zote za nchi yetu ambayo pamoja na utajiri wake wa rasili-mali na watu ni moja kati ya nchi maskini sana duniani.

Mwisho.

MAENEO YA KUMULIKWA 2012

Na Ezekiel Kamwaga

MWAKA jana yaani 2011ulikuwa ni mwaka ambao habari nyingi kuhusu rushwa ziliandikwa katika vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini.na kwa kiasi kikubwa zilitikisa Taifa kwa kuathiri uchumi wetu najamii yetu.
Kama ilivyo ada, jarida hili la **Kurunzi ya Ufisadi lilikuwa mstari wa mbele katika kufanya uchunguzi** wa kina kuhusiana na rushwa hapa nchini.

Katika toleo hili la kwanza kwa mwaka huu wa 2012, tumefanya uchunguzi na kubaini maeneo mbalimbali ambayo ni lazima vyombo vya usalama viyafanyie kazi kubwa na mapema iwezekanavyo ili kuhakikisha Mianya ya vitendo vya rushwa vinaepukika na kuzuiliwa.

Maana ya kufanya kazi hii ni kwamba, si tu, kila siku tuishie kuandika taarifa za vitendo vya rushwa ambavyo vimefanyika tayari ,lakini pia kubainisha maeneo ambayo kama umakini utakuwapo, rushwa inaweza kudhibitiwa.

Yafuatayo ni maeneo ya hatari kwa rushwa mwaka huu wa 2012.

Uchaguzi Mkuu wa CCM

HUU ni mwaka wa uchaguzi kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Uzoefu unaonyesha kuwa chaguzi nyingi ambazo zinakuwa zikifanyika ndani ya vyama vya siasa hutawaliwa na rushwa,lakini uchaguzi wa chama tawala huwa ni hatari zaidi
Jambo la kukumbuka hapa ni ukweli kuwa uchaguzi wa CCM mwaka huu una nafasi kubwa ya kutoa mwelekeo wa nani au akina nani watabeba bendera ya chama hicho kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Kutakuwa na uchaguzi wa wajumbe wa Halmashauri Kuu (NEC) ya chama hicho na wale wa Mkutano Mkuu wa CCM. Vyombo hivi vyote vina ushawishi mkubwa katika maamuzi yanayofikiwa na chama hicho kikongwe katika siasa za hapa nchini..

Katika uchaguzi wa mwisho wa namna hii ndani ya CCM, ziliibuka tuhuma mbalimbali za rushwa miongoni mwa wagombea wa nafasi hizo,suala lililo pelekeauongozi wa chama hicho kuagizaTaasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuingilia kati na kuchunguza tuhuma hizo.

Kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka juzi yaani 2010, wagombea watatu ambao ni wanasiasa maarufu waliowania uteuzi ndani ya Chama chao katika nafasi ya ubunge, akiwemo aliyekuwa Waziri katika awamu ya tatu nay a nne,Mh , Joseph Mungai, walifikishwa mahakamani kwa tuhuma za rushwa ya uchaguzi.

Jambo pekee la kutilia maanani ni kuwa katika uchaguzi huo wa mwaka 2010, wagombea pekee waliofikishwa mahakamani walikuwa ni wale wa CCM na si wa vyama vingine vya siasa hapa nchini.

Hili halimaanishi kuwa wagombea wa vyama vingine hawakutoa rushwa, ila inaonyesha namna tatizo hilo lilivyo kubwa ndani ya CCM.

Wafanyabiashara wakubwa wa makampuni yenye maslahi na utawala wa sasa, yanafuatilia kwa makini mchakato na mwenendo wa uchaguzi huo ,na huwa tayari kuingia makubaliano ya namna ya kuwafadhili rasilimali mbalimbali zikiwemo fedha wanasiasa hao , ambao huahidi kulinda maslahi ya biashara zao mara wafanikiwapo kuingia madarakani.

Ingawa duru za kisiasa hazitabiriki na hubadilika wakati wowote, wachambuzi wengi wanaamini kuwa bado atakayekuwa mgombea wa CCM ndiye atakayekuwa na nafasi kubwa ya kushinda katika uchaguzi ujao wa mwaka 2015.Na hii itatokana na aina ya wajumbe watakaochaguliwa ,na mahusiano yao na wagombea wanaotajwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini kwenye nafasi hiyo iliyo nyeti kwa Taifa.

Katika taifa ambalo lina tatizo kubwa la fedha haramu, wafanyabiashara wakubwa wa dawa za kulevya, mikataba isiyoeleweka katika sekta za nishati na madini na fursa ya kutengeneza fedha nyingi kwa wanasiasa, uchaguzi wa CCM una kila dalili mwaka huu. Kurunzi ya Ufisadi linataraji vyombo husika vitafuatilia kwa karibu kila kinachoendelea na kudhibiti mianya na vitendo

na vitnedo vyote ya Rushwa ilikupata viongozi waadilifu.



Halmashauri kuu ya CCM (NEC)

Mkataba wa IPTL

Miongoni mwa mikataba ya hovyo kabisa kuingiwa na serikali ya Tanzania ni mkataba huu wa IPTL wa mwaka 1995.

Kampuni hii iliingia mkataba wa miaka 20 wa kuzalisha umeme kwa serikali ya Tanzania, huku ukipingwa na wabunge na taasisi za kimataifa kama vile Transparency International (TI) kwa sababu ya matatizo mbalimbali yaliyoonekana katika siku za mwanzo kabisa.

Kwanza mitambo hiyo ya IPTL ilikuwa inatumia mafuta jambo lililoonekana mapema kuwa litaisababishia serikali ya Tanzania hasara kubwa kutokana na gharama za juu za nishati hiyo

Kulikuwa pia na tatizo la tozo kubwa ya gharama za uendeshaji za mitambo hiyo ambapo serikali kupitia TANESCO ilitakiwa kulipa walau Sh bilioni nne kila mwezi kwa IPTL hata kama haikununua umeme wowote wakati huo.

Mpaka miaka mitano iliyopita, serikali ilikuwa imelipa walau Sh bilioni 160 za kitanzania kama malipo ya gharama za uendeshaji pekee ukiondoa zile kubwa zaidi za kulipia umeme wenyewe,

Hata hivyo, hivi karibuni, serikali imebaini kuwa imepoteza kiasi cha dola 54 milioni za Marekani (Sh bilioni 86) kutokana na watendaji wake kutoa hesabu za uongo kwenye ununuzi wa mafuta ya kuendeshea mitambo ya IPTL.

Kiongozi mmoja wa juu wa Wizara ya Nishati na Madini ameliambia jarida hili kwa masharti ya kutotajwa jina kwamba kwa kawaida ‘dili’ za ununuaji wa mafuta hufanywa na mtandao maalumu wa watendaji na hivyo kuna watu wengi watabainika.

“Kuna mtandao mkubwa wa watendaji ndani ya wizara na nje ambao wananufaika sana na ununuaji wa mafuta. Kama uchunguzi utafanyika vizuri, kuna vigogo wengi wataumbuka. Subirini tu mtasikia mengi,” kilisema chanzo hicho.

Chanzo hicho kililiambia jarida hili kuwa ingawa wananchi wamekuwa wakipigia kelele mkataba huo wa IPTL kwa muda mrefu,bado haikuwezekana kuchukua hatua za kiuchunguzi kwa sababu kuna watu wamekuwa wakifaidika sana na mkataba huo.

Ni matarajio ya jarida hili kuwa uchunguzi huo wa wizara utakapokamilika, Watanzania watasikia mengi kutoka huko.

Ufisadi kwenye Halmashauri


.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Aggrey Mwanri, amefanya ziara nyingi katika Halmashauri mbalimbali nchini na kile kinachoandikwa kwenye vyombo vya habari kinatoa picha mbaya kwa Serikali,ambayo inapelekea takribani nusu ya mapato yake kwenye Halmashauri zake, ufisadi unaofanyika kwenye halmashauri nyingi unaonyesha kuwa hali si shwari.

Shule zinazojengwa hazina viwango vya gharama zinazodaiwa kutumika, kuna mamia ya watumishi wengi hewa, barabara hazina viwango vya gharama zilizotumika na fedha zinatumiwa vibaya pasipo kufuta sheria na taratibu zinazotawala Manunuzi ya Umma hapa nchini.

Tayari Mwanri ametangaza bungeni kuwa atakula ‘sahani moja’ na viongozi au watumishi wa halmashauri watakaobainika kufisadi mali za umma.

Ni wazi kuwa tutayasikia mengi kutoka kwenye halmashauri zetu mwaka huu wa 2012. Tutege masikio.



Waziri wa nishati na madini
Mhe. William Ngeleja

Sh trilioni 1.7 za umeme wa dharura

Katika bajeti ya mwaka huu wa 2011/2012, serikali imetenga kiasi cha Sh trilioni 1.7 kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la umeme linalo likabili Taifa.

Hata hivyo, uzoefu umeonyesha kwamba sekta ya nishati imekuwa ikitawaliwa sana na ufisadi hususani inapokuja kwenye uingiaji wa mikataba na wale wanaotakiwa kuiuzia serikali umeme.

Maswali mengi yameanza kuzuka juu ya kiwango hicho cha fedha. Mbunge wa Kigoma Kaskazini (Chadema), Zitto Kabwe, tayari ameweka wazi msimamo wake kuwa kiasi hicho cha fedha ni kikubwa sana huku tija ikiwa ni ndogo.

Kwa mfano, Zitto amenukuliwa akihoji juu ya kiwango hicho cha fedha kwamba kingeweza kabisa kutumika kutengeneza bomba la gesi kutoka Mnazi Bay, Mtwara kwenye hazina kubwa ya gesi hadi Dar es Salaam .
Kwa uzoefu ambao taifa hili inao kwenye sekta ya nishati, ni wazi kuwa kuna habari nyingi tutaanza kuzikia hivi karibuni kuhusiana na matumizi ya fungu hilo kubwa la fedha.

Hili ni eneo ambalo yatasikika mengi sana mwaka huu.

Mwisho.

Rushwa inapenyezwa sehemu takatifu?

Na Ezekiel Kamwaga

WAKATI watu wanaotajwa kutaka kuwania nafasi za juu kisiasa hapa nchini wakipishana kutoa misaada katika vyombo vya kidini, hofu imetanda kuhusu uwezekano wa rushwa sasa kuanza kupenya katika “sehemu takatifu.”

Tangu mwishoni mwa mwaka jana, vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini vimekuwa vikiripoti kuhusu namna wanasiasa wanavyopishana kwenye makanisa na misikiti kwa ajili ya kusaidia masuala mbalimbali.

Jarida hili limeambiwa kuwa baadhi ya wanasiasa sasa wamekuwa “lulu” makanisani kiasi kwamba wamepokea mialiko mingi na hawawezi kupokea mwaliko mpya kwa vile ratiba zao zimejaa hadi katikati ya mwaka huu.

Ingawa mwanzoni michango hii ilikuwa ikionekana kuwa ya kawaida, hali ilianza kubadilika baada ya kutolewa kwa matamko yaliyozua maswali kutoka kwa wanadini wenyewe na wanasiasa wanaotajwa kujihusisha na michango hiyo.

Kwa mfano, Askofu wa Kanisa la Anglikana jimbo la Dar es Salaa, Dk. Valentino Mokiwa, aliwahi kunukuliwa akimwambia Waziri Mkuu wa zamani, Edward Lowassa, kuwa amkumbuke katika “ufalme wake.”

Kwa sasa, Lowassa hana wadhifa wowote zaidi ya ubunge na Uenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Hata hivyo, jina lake ni miongoni mwa yale yanayotajwa sana kwenye kinyang’anyiro cha kuwania urais kupitia CCM mwaka 2015.

Lowassa alikuwa miongoni mwa wachangiaji wakuu katika sherehe za kuchangia kanisa hilo la Anglikana mwaka jana na hatua ya Mokiwa kuomba yeye na kanisa lake wakumbukwe na mwanasiasa huyo ilimaanisha kwa wengi kuwa anafahamu kiongozi huyo atagombea.

Zaidi ya Lowassa, majina mengine ya wanasiasa wanaotajwa kusaka urais kwa kupitia migongo ya kidini ni Samuel Sitta, Frederick Sumaye na Benard Membe.

Ingawa Katiba ya Tanzania haisemi chochote kuhusu dini ya mgombea urais, kuna uwezekano mkubwa kwamba mgombea urais ajaye kupitia CCM atatoka katika dini ya kikristo kwa vile rais aliyepo sasa ni Muislamu.

Wachunguzi wa masuala ya kisiasa wanadai kwamba ukweli huo ndiyo unaowafanya wanasiasa kuamua kutumia makanisa kisiasa kwa vile mgombea mkristo anayeungwa mkono na makanisa ana nafasi kubwa ya kuwa Rais.

Hata hivyo, Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Issa bin Shaaban Simba, amekana michango inayotolewa kwa taasisi za kidini kufungamanishwa na mbio za urais mwaka 2015.

“Wanasiasa hawahitaji makanisa wala misikiti kushinda. Kwa sisi wenye umri mkubwa, tumeshuhudia kwa macho yetu wakristo wakishiriki kwenye shughuli za ujenzi wa misikiti katika miaka ya nyuma.

“Tatizo ninaloliona sasa ni kuwa vyombo vya habari vimekuwa vingi mno kiasi kwamba kila kidogo kinachofanyika kinaandikwa magazetini na redioni. Hali haikuwa hivi zamani,” alisema kiongozi huyo wa Waislamu nchini.

Alisema Watanzania hawawezi kumchagua mtu eti kwa kuwa anasaidia sana misikitini na makanisani na kwamba wanasiasa wanalijua hilo fika.

“Mimi binafsi, itakapofika siku ya kufanya uchaguzi, sitachagua mtu kwa sababu alijenga misikiti mingi. La hasha. Nitachagua yule ambaye nitaona anafaa kuwa kiongozi mkuu wa nchi au jimbo,” alisema.

Hata hivyo, muumini wa Kanisa la Full Gospel Bible Fellowship (FGBF), Terevaeli Kanuya, alisema kuna dalili za rushwa kuwa kichocheo cha misaada mingi inayotolewa na wanasiasa kwenye taasisi au vyombo vya kidini.

“Kama utaangalia kwa makini, wafaidikaji wakuu wa michango hii ni makanisa makubwa. Wakatoliki, Waanglikana na Walutheri ndiyo wanaopata misaada zaidi kuliko makanisa ya Pentekoste. Hii yote ni kwa sababu makanisa haya ni makubwa zaidi na yana mfumo unaoeleweka wa kupeleka taarifa,”alisema.
Jambo linalosababisha kuenea kwa hisia hizi za rushwa katika sehemu takatifu ni hatua ya wanasiasa wenyewe kutuhumiana kwenye kwa jambo hilo.

Akizungumza mkoani Arusha mwaka jana, Sitta alidai kuwa baadhi ya wanasiasa ambao wanafahamika kuwa si wasafi, wameamua kutumia makanisa na misikiti kujisafisha kwa kutoa misaada.

Kauli hii ilitafsiriwa kuwa ni vijembe kwa wanasiasa wengine ingawa hata naye anadaiwa na wanasiasa wenzake kuwa michango yake mingi kwenye taasisi za kidini ina malengo ya kisiasa.

Akizungumzia hisia hizi za rushwa, Ofisa Habari wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Doreen Kapwani, alisema ni vigumu kuhusisha michango hii na vitendo vya rushwa.

Alisema katika hali ya kawaida, rushwa huwa ni suala la siri kubwa na ni watu wachache sana hupata nafasi ya kujua undani wake. Katika hali hiyo, Doreen alisema ni vigumu kuhusisha rushwa na michango ambayo watu huitoa hadharani.

“Kama utafanya utafiti wa kutosha, utabaini kwamba wanasiasa hao huwa wanaalikwa na makanisa au misikiti kwenye shughuli zao. Siwezi kutetea moja kwa moja lakini kama suala hilo litafika mezani kwetu katika namna unayoisema, tutalifanyia kazi,” alisema.

Hata hivyo, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) Dar es Salaam, Frank Sanga, anasema ni muhimu sana kwa vyombo vya dola kuchunguza suala hili kwa vile inaonekana kabisa michango si ya kawaida.

“Kuna maswali mengi ya kujiuliza kuhusu hali hii. Kwamba mbona spidi ya kuchangia imekuwa kubwa? Mbona wahusika ni wale wale kila siku? Wachangiaji hawa wamepata wapi ukwasi wa kuwawezesha kuweza kuchangia mamilioni kila wiki?” alihoji.

Hata hivyo, mlei wa Kanisa Katoliki Kijichi, John Kamala, alisema ni vema Watanzania wenye uwezo wakaachwa wachangie dini zao kwa vile ndiyo namna pekee itakayowezesha maisha ya kidini kushamiri.

Zamani, wafadhili wetu wakuu walikuwa ni wazungu. Kwa bahati mbaya hali nyao ya kiuchumi kwa sasa ni mbaya. Hii maana yake ni kwamba makanisa yetu inabidi yatafute wafadhili wa ndani ili kufanya mambo yake.

“Sasa kama wafadhili wenyewe ni wanasiasa, basi hatuwezi kuwakataza. Hakuna tofauti ya kukataa fedha za mwanasiasa lakini ukapokea fedha za mashoga na wauza unga na silaha. Tuwaache watu hawa watuimarishie taasisi zetu,” alisema Kamala.

Kinondoni: Huduma za Afya Zazorota katika Lindi la Utajiri.

Na Emanuel Adamson

.

WILAYA ya Kinondoni jijini Dar es Salaam ndiyo inayoongoza kwa wingi wa vyanzo vya mapato. Ndiyo wilaya ambayo watu wengi wenye vipato vikubwa na mamlaka makubwa serikalini wanapoishi.

Hata hivyo, pamoja na yote hayo, ndiyo wilaya ambayo pengine ina huduma mbovu zaidi za afya miongoni mwa Halmashauri zote zinazounda jiji la Dar es Salaam, uchunguzi wa *Corruption Almanac* umebaini.

Hali hii mbaya ya upatikanaji wa huduma za afya ipo katika ngazi zote kuanzia zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali zilizo chini ya umiliki wa serikali.

Mfano hai wa hali hii mbaya ya upatikanaji wa huduma za afya ni Kata ya Manzese. Uchunguzi wa Kurunzi ya Ufisadi umebaini kuwa kata hii yenye mitaa saba na miongoni mwa maeneo yenye idadi kubwa ya watu si Kinondoni pekee bali Dar es Salaam kwa ujumla, haina kituo cha afya, zahanati wala hospitali ya serikali.

Kutokana na wingi wa watu wanaoishi Manzese, kata hiyo ni miongoni mwa waathirika wa magonjwa ya mlipuko; na ndiyo maana inashangaza kuwa serikali haijaweka hata kituo chake cha afya katika eneo hilo.

Watafiti na wananchi waliozungumza na jarida hili wameeleza kushangazwa kwao na vigezo vinavyowekwa na serikali kwenye kuamua wapi kujengwe kituo, zahanati au hospitali ya serikali.

Jarida hili limebaini pia kuwa umuhimu wa huduma ya afya kutoka serikalini katika kata ya Manzese ni mkubwa kwa vile wengi wa wananchi wake wana vipato vya chini na hivyo uwezo wao ni kupata huduma zilizo na ruzuku kutoka serikalini.

Jarida hili limebaini pia kuwa hali hiyo ndiyo imekuwa chanzo kikubwa cha kushamiri kwa vitendo vya rushwa, unyanyasaji na kero katika maeneo mengi ambapo huduma za afya kutoka serikalini ni adimu.

Katika kuangalia hali ya upatikanaji wa huduma za afya katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, jarida hili limefanya utafiti wake katika kata tatu za manispaa hiyo ambazo ni Manzese, Goba na Mwananyamala.

Hali ambayo utafiti wetu ulikutana nayo katika maeneo hayo yanatia shaka dhamira ya serikali ya kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Tofauti na Manzese, walau Goba na Mwananyamala wana hospitali na vituo vya afya vya serikali. Lakini,



Hali ya wagonjwa katika wodi ya akina mama katika Hospitali ya Mwananyamala

hapa pia linaibuka tatizo lingine –ubora wa huduma zenyewe zinazotolewa.

Kwa mfano, wakazi wa Goba wanafananisha huduma wanayoipata katika zahanati yao na hospitali zingine, kwamba hazitofautiani na zile walizokuwa wanazipata kwa waganga wa kienyeji (tiba za jadi) kwamba mganga wa jadi humpima mgonjwa kwa kumwangalia na kumpa dawa, suala ambalo hata Zahanati ya Goba wanafanya.

Hawapati vipimo vya kisayansi, zaidi ya daktari kukuangalia usoni na kukutajia ugonjwa na dozi ya dawa mseto.

Katika mahojiano na wakazi wa Goba, jambo kubwa lililozungumzwa lilikuwa ni ukosefu mkubwa wa maadili miongoni mwa wauguzi wanaofanya kazi zao katika zahanati hiyo.

Kijana mmoja ambaye hakutaka kutaja jina, alitoa ushuhuda wa namna alivyompoteza mtoto wake kichanga katika zahanati ya Goba kwa sababu tu ya unyama na ukosefu wa weledi kutoka kwa muuguzi wa zamu siku hiyo.

“Mke wangu alikwenda pale kujifungua usiku. Tuligonga sana mlangoni mwa muuguzi lakini hakufungua mlango wake. Matokeo yake mke wangu akajifungua palepale mlangoni mwa chumba cha muuguzi. Miye nikageuka kuwa mkunga”.

“Ndipo muuguzi alipotoka chumbani kwake kwa kujikongoja na akamchukua mtoto bila hata ya kumfunika kama ilivyo ada. Nashukuru mama wa mtoto alipona lakini mtoto alifariki siku hiyo hiyo,” alisema kijana huyo aliyejitambulisha kama mjasiriamali.

Wengi wa wananchi pia walikubaliana na maoni ya

wengine kuwa hakuna vipimo vyovyote vinavyopimwa kwa mgonjwa ili apate tiba kutokana na ubainiji wa kipimo. Walishindwa kutofautisha huduma ya afya ya kitaalamu na ile huduma ya afya ya jadi.

Wanasema "Serikali inasisitiza kwamba tuachane na tiba za jadi na kutusisitiza kwamba tuende kwenye vituo vya afya, huku ikidhani kituo cha afya ni majengo na wauguzi tu, kumbe sivyo, mbona tukienda pale zahanati daktari anakutazama usoni, ataweka mkono wake shingoni, atakuambia unaumwa malaria na kukuandikia dozi ya dawa mseto pasipo kupata vipimo vya maabara, sasa kunatofauti gani na waganga wa jadi na hawa wa hospitalini?maana wa jadi anakutazama na kukupa dozi," wanahoji.

Wakati yote haya yakijiri katika zahanati ya Goba,hali haijawa shwari kwa Hospitali ya Mwananyamala yenye historia mbaya katika utoaji wa huduma bora kwa wagonjwa wanaofika hospitalini hapo.

Jarida hili lilipofanya mazungumzo na watumiaji wa hospitali hiyo, akiwemo wakazi wa Mwananyamala na waliweza kuzungumzia ukimya wa vyombo vinavyoisimamia hospitali hiyo kutokana na mengi yanayosemwa katika vyombo vya habari, lakini hakuna mabadiliko katika uboreshaji wa huduma katika hospitali hiyo kubwa na inayotegemewa na wakazi wengi wa Dar es Salaam.

Jarida hili lilipofanya mahojiano na dada mmoja ambaye ni mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Msisiri kata ya Mwananyamala na alianza kwa kusema.

"Kinachosemwa kwenye vyombo vya habari kuhusu hospitali ya Mwananyamala ni kidogo kuliko ukienda kushuhudia madhambi ya hospitali hii wewe mwenyewe. Kwani rushwa, dharau na matusi vimetawala kwa wauguzi.

"Ukiingia kule wodi ya wazazi, kama una uchungu ukifika huko damu zimetapakaa juu ya vitanda, mpaka zingine zimegandamana vitandani. Wakati mwingine unakuta mwenzako ametoka kujifungua ndani ya nusu saa iliyopita na hakuna usafi uliofanyika. Unaambiwa tandika kanga yako hapo juu ya damu na lala tukuhudumie".

"Unalala juu ya damu, sasa hawa ndiyo wanaosimamia afya zetu na kutusisitiza usafi? Usafi uko wapi katika sehemu nyeti kama hizi? vipi kuhusu magonjwa ya kuambukizana kupitia damu"alihoji dada huyo huku akionekana wazi kuwa na hasira.

Wanahoji pia juu ya bajeti ya Serikali kwamba inakuwa inakwenda wapi wakati kila mwaka huwa tunaskia mabilioni ya Shilingi yakiwa yametengwa katika sekta hiyo ya afya.

Akizungumzia hali hii, Mratibu wa Huduma za Afya katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Dk. Zainab Majapa, amekiri kuwapo kwa changamoto hizi zilizoibuliwa na wananchi ambao ndiyo watumiaji wakuu wa huduma hizi, lakini amewarushia lawama kuwa ni wavivu katika kutoa ushirikiano pale panapobainika kuwapo kwa harufu ya rushwa kati ya daktari na mgonjwa.

Dk. Majapa alitoa lawama hizo huku akielezea uzoefu wake katika hospitali tofauti za manispaa hiyo ambapo akiwa mkuu wa vitengo mbalimbali alijitahidi sana katika kukomesha rushwa katika utoaji huduma, ambapo wagonjwa walikuwa wakimficha kwa kumnyima ushirikiano.

Mwisho.

Integrity Watch Yazindua Mradi wa Afya

TAASISI ya Integrity Watch ambayo pia ndiyo wachapishaji wa jarida hili la *Corruption Almanac*, limezindua mradi wa kuboresha upatikanaji wa huduma za afya katika kata tatu za Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

Uzinduzi huo ulifanyika Februari 25 mwaka huu katika Hoteli ya Top Life iliyopo jijini Dar es Salaam huku mgeni rasmi akiwa ni Diwani wa Kata ya Ndugumbi, Lucas Mgonja, aliyemwakilisha Mstahiki Meya wa Kinondoni.

Lengo la Mradi huu wa Integrity Watch ni kuwapa wananchi uwezo wa kufahamu haki na wajibu wao kwenye kuhakikisha wanapata huduma bora za afya katika vituo vinavyohudumiwa na serikali.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi hiyo, John Jingu, alieleza kuhusu wajibu wa kuiwezesha jamii kama mdau muhimu katika sekta ya afya,katika kujua na kufahamu wajibu wake kama jamii kwa maana ya sera na uendeshwaji mzima wa sekta hii muhimu, kwamba jamii ikipewa uwezo basi hata vitendo vya rushwa vitapungua kwa kiasi kikubwa.

Mwisho

KUTOKA MAGAZETINI.

Wabunge Waagiza Fedha za Maafisa Zikaguliwe.

Kamati ya kudumu ya Bunge ya hesabu za Serikali [PAC],Imesema matumizi ya fedha za misaada zinazotolewa kupitia kitengo cha maafa hayaeleweki na kuagiza kufanyika ukaguzi wake kuanzia milipuko ya mabomu ya mwaka jana Mbagala,Gongolamboto na mafuriko ya mvua mwaka huu.
[Nipashe,Mtanzania,Mwananchi 16/02/2012]

Madiwani Magu wakerwa wizi dawa za Serikali.

Madiwani katika Halmashauri ya Magu mkoani Mwanza,wamekerwa na wizi wa dawa zinazotolewa na Serikali uliotokea katika hospitali ya wilaya ya Magu,unao muhusisha mganga wa kituo cha ugalukilo,Dk Kija Makwani.Madiwani hao walikerwa na kitendo hicho wakati wakijadili wizi huo wa dawa aina ya Mseto katika kikao chao kilichofanyika mjini hapa hivi karibuni.
[Mtanzania 16.02.2012]

PAC yabaini madudu Maliasili.

Madudu ya kihasibu ambayo yameendelea katika wizara ya Maliasili na Utalii yamesababisha wizara hiyo kuendelea kuibuka na hati chafu toka ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali[CAG] ,kwa miaka mitatu mfululizo.
Madudu hayo ambayo yanahusu wizara kutokuwa na daftari la kudumu la kutunza takwimu za watalii wanaoingia nchini na wawindaji wanaoendesha shughuli zao katika maeneo ya uwindaji,yamesababisha CAG ashindwe kupata takwimu sahihi kukaagua kile kinachoingizwa na wizara kama pato la nchi,aidha madudu mengine ni kukiukwa kwa sheria ya fedha inayotaka fedha zote zinazokusanywa na vyanzo mbalimbali vya Serikali kupelekwa kwanza hazina ili zikaingizwe kwenye vitabu vya Serikali kisha kurejeshwa kwenye vyanzo ambavyo hutakiwa kubakiwa na sehemu ya fedha zilizokusanywa.

Vigogo TRA Sirali wasimamishwa kazi.

Maofisa watatu wa kituo cha forodhani Sirari cha Mamlaka ya Mapato Tanzania Mkoani Mara,wamesimamishwa kazi kwa tuhuma mbalimbali ikiwemo ya kula njama na wafanyabiashara kukwepa kulipa ushuru wa Mapato.Meneja wa Mapato Tanzania[TRA] mkoani Mara Mrasoni Msangi alisema maafisa hao wamesimamishwa kutokana na kukiuka maadili ya kazi baada ya kushirikiana na wafanyabiashara kukwepa kulipa mapato.
Maafisa hao walikuwa wanakula njama za kukwepa kulipa ushuru na wafanyabiashara wakubwa wanaoingiza bidhaa zao nchini kutoka nchi za Dubai,China na Kenya.Inadaiwa maafisa hao katika kufanikisha njama hizo wamepandikiza mawakala bandia katika kampuni za Clearing Agent zilizopo katika mji mdogo wa Sirali.
[Nipashe 20/02/2012]

Ofisa Uvuvi kortini kwa Rushwa.

Taasis ya kuzuia na Kupambana na Rushwa [TAKUKURU] Mkoani Kagera imempandisha Kizimbani afisa uvuvi Utawala na doria Mkoani Kagera,Bilali Banal kwa Makosa ya Kuomba na kupokea Rushwa kutoka kwa wavuvi wa Ziwa Viktoria.
Alisema katika kosa la kwanza mtuhumiwa anadaiwa kuomba Rushwa y ash 600,000 kutoka kwa Bazil Juma Thadeo baada ya kukomata boti yake na zana za uvuvi.Katika kosa la pili mtuhumiwa anadaiwa kupokea Rushwa y ash 500,000 baada ya TAKUKURU kumwekea mtego.
[Tanzania Daima 03/03/2012]

Mataka aongezewa mashitaka.

Upande wa Jamhuri katika kesi ya matumizi mabaya ya ofisi ya umma na kusababishia hasara, Aliyekuwa mkurugenzi Mtendaji wa shirika la ndege la Tanzania(ATCL) David Mattaka na wenzake umeongeza mashtaka ya washtakiwa hao. Wakili Kimaro alidai kuwa shitaka la kwanza linawakabili washitakiwa wote watatu ni la kula njama kinyume na kifungu cha 32 cha sheria ya kuzuia na kupambana na Rushwa Na.11 ya Mwaka 2007 ambapo Mataka na wenzake katika tarehe tofauti Machi –Julai 2007 Jijini Dar ES Salaam ,walikula njama na watu wengine wasiojulikana kutenda kosa la matumizi mabaya ya Ofisi ya Umma, kutumia madaraka yao vibaya kwa kuidhinisha ununuzi magari 26 yaliyotumika kitendo ambacho ni kinyume na kifungu cha 31 cha Sheria ya manunuzi ya umma Na.21 ya mwaka 2008 pamoja na kanuni zake zilizotengenezwa na sheria hiyo. Shitaka la tatu ni matumizi mabaya ya Madaraka kwa kuagiza magari hayo ya mitumba bila kutangaza tenda ya ushindani na kuyanunua kwa thamani ya dola za kimarekani 809,000 kutoka kampuni ya 3 IN DALIMOUK MOTORS ya Dubai katika Jamhuri ya Emirates,kinyume na kifungu cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2008 na kanuni zake.
[Tanzania Daima,Nipashe, Mwananchi 17/03/2012]

Mabilioni ya Rada yarejeshwa rasmi nchini.

Maandalizi ya marejesho ya [aundi 29.5 Milioni sawa na 80 bilioni, zinazotokana na ununuzi wa Rada baada ya Tanzania na Uingereza kutiliana Saini makubaliano ya kurudisha'' chenji'' hiyo.
Kwa mujibu wa makubaliano hayo yaliyofikiwa jana nchini Uingereza, fedha hizo sasa zitaingizwa Benki kuu ya Tanzania [BOT] wakati wowote na kutumika kwa ununuzi wa madawati na vitabu kwajili ya shule za msingi. Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU amenukuliwa akisema kuwa hakuna Mtanzania aliyepatikana na makosa ya rushwa kwenye sakata la Rada.
[Mwananchi 16.03.2012]

TAKWIMU KUHUSU RUSHWA KUTOKA TAKUKURU

1995 -2011

YEARS	Allegations received	Cases Investigated	Completed Investigation files	Administrative actions taken	Files transferred to other agencies	New cases into courts	Total cases Prosecuted	Conviction cases	Acquittal cases	Saved Money/ Asset recovered
1995	261	261	145	-	-	8	16	1	7	2,706,800,000/=
1996	513	513	245	-	-	21	34	2	9	1,900,651,000/=
1997	510	510	289	-	-	9	18	1	4	6,932,950,000/=
1998	545	545	200	-	95	15	31	2	6	9,300,478,000/=
1999	1,116	1,116	304	-	209	62	47	9	25	14,795,169,650/=
2000	1,244	1,244	276	-	234	49	42	6	3	11,100,000,000/=
2001	1,354	1,354	285	1	154	57	53	-	-	2,500,000,000/=
2002	1,383	1,383	732	42	222	52	191	12	12	2,714,199,000/=
2003	2,285	1,796	540	21	36	51	178	9	28	3,800,266,000/=
2004	2,223	1,149	458	126	25	60	202	6	8	4,000,216,000/=
2005	3,121	677	540	111	2	50	218	6	10	2,500,600,000/=
2006	6,320	1,528	1,688	209	496	71	251	18	28	1,301,492,528/=
2007	8,235	1,266	2,015	280	460	196	352	35	45	1,580,099,081/=
2008	6,137	928	936	74	184	147	416	37	71	13,203,459,357/=
2009	5,930	884	1,175	40	152	222	463	46	73	436,132,336/=
2010	5,685	870	924	29	135	224	587	64	98	10,123,258,300/=
2011	4,765	819	773	30	84	193	466	52	61	4,638,939,558/=
TOTAL	51,627	16,843	11,525	963	2,488	1,487	3,565	306	488	93,534,710,810

Source: PCCB HQ, January 2012.

Kurunzi ya IWa

Taarifa za Rushwa -65

Taarifa zilizoshughulikiwa -2

Taarifa ambazo hazijashughulikiwa-62

ORRUPTION ALMANAC

Stamp Out Corruption, Be a Part of the Battle

Hanns Seidel Foundation

IWa

Contact us

Tel: +255 612 253545

Email: info@integrity-watch.com

webbsite: www.integrity-watch.com